## Shughuli Zinazofanywa na Asasi

1. Kutoa Elimu ya mahusiano na Stadi mbalimbali za maisha kwa wanafunzi wa shule na vyuo.
2. Kutoa ushauri na unasihi wa kisaikolojia na kimahusiano kwa watoto, vijana, wanandoa, wazazi wasio na wenza, familia na mtu mmoja mmoja.
3. Kuandaa na kufanya semina na makongamano ya makundi rika jinsi ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, unyanyasaji, mimba na ndoa za utotoni.
4. Kufanya tafiti, Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vielelezo na machapisho mbalimbali yenye lengo la kuelimisha jamii kuhusu ndoa na familia, malezi, haki za wanawake na watoto.
5. Kutoa Mafunzo mahsusi kuhusu Taasisi ya Ndoa kwa Wanandoa na Vijana wa Kike na Kiume wanaotarajia kuingia katika ndoa.
6. Kutoa msaada wa Kisaikolojia, elimu ya uzazi, malezi na ujasiriamali kwa wazazi wasio na wenza, hasa wanaoishi katika mazingira magumu
7. Kutoa mbiu shawishi (advocacy) kwa serikali na vyombo mbalimbali vinavyohusika ili kufanya maboresho katika Sheria, Sera, na Miongozo kwa lengo la kuimarisha ndoa, familia na malezi ya watoto.
8. Kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, Halmashauri, Mkoa na Taifa zinazohusiana na malengo ya Asasi.

## Msingi wa Huduma za Asasi

+ TaMCare ni Asasi isiyotengeneza faida. Inatoa huduma zake kwa jamii bila malipo.
+ Mtu yeyote anayeguswa na huduma zetu, anaruhusiwa kutoa mchango wake wa hisani kwa hiari ili kuimarisha huduma za Asasi hii.




**Kwa Mafunzo, Ushauri na Unasihi**
**Wasiliana Nasi:**
Asasi ya Ndoa na Malezi ya Watoto Tanzania (TaMCare)
S. L. P 185, Bagamoyo, Tanzania
**Simu:** +255 744 000 066
**Barua Pepe:** info@tamcare.or.tz
**Tovuti:** www.tamcare.or.tz


# KUHUSU ASASI YA TaMCare

# Utangulizi

- Ndoa ni taasisi nyeti na muhimu katika maisha ya binadamu. Ni Taasisi muhimu katika Nyanja zote za dini, jamii, serikali na siasa. Bila kuwa na ndoa nzuri na imara, dini, jamii, serikali na hata siasa vitayumba na kukosa maadili mema, haki, utulivu, na amani miongoni mwa watu.
- Ni jambo la kusikitisha kuwa, watu wengi wanaichukulia taasisi ya ndoa kwa wepesi. Watu hawajiandai ipasavyo kwa ajili ya maisha ya ndoa. Matokeo yake ni mpasuko na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Hali hii ni sehemu ya visababishi vya ongezeko la wazazi wasio na wenza (single parents) nchini.
- Hii ni changamoto kubwa inayoikabili nchi yetu. Athari zake ni kubwa kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo, wazazi wenyewe, jamii na Taifa kwa Ujumla. Ongezeko la watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu, watoto waliokosa maadili mema, walioacha shule, walioathirika kiafya na kisaikolojia, waliojiingiza katika vitendo vya uhalifu kama vile kula madawa ya kulevya, umalaya, ujambazi na makosa mengine ya kijinai ni sehemu ya matokeo ya hali hii.
- Ndoa ni kitovu cha malezi na ustawi wa jamii na Taifa. Hivyo, ili kuwa na jamii na Taifa lenye ustawi na maendeleo ni muhimu Ndoa kuwa imara na zenye furaha. Ndoa zisizo na furaha, huathiri afya ya mtu binafsi, ustawi wa familia, jamii na ufanisi katika utendaji kazi.



# TaMCare ni nini?

Asasi ya Ndoa na Malezi kwa Watoto Tanzania, yaani Tanzania Marriage and Child Care Foundation, kwa kifupi TaMCare. Ni Asasi isiyo ya Kiserikali na isiyotengeneza faida yenye makazi yake Wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani katika Tanzania Bara. Asasi hii imesajiliwa na Serikali Mwezi Oktoba mwaka 2019. Namba yake ya usajili ni 00NGO/R/0717.

TaMCare inagusa kiini cha maisha ya mwanadamu. Inahusika na masuala ya ndoa na watoto bila kujali dini, kabila, rangi, wala jinsia.

## Dira yetu

Kuwa taasisi bunifu na inayoaminika katika kuchangia uwepo wa jamii bora inayotokana na ndoa imara na malezi bora kwa watoto.

## Dhima yetu

Kutoa huduma bora na endelevu kuhusu ndoa na malezi bora kwa watoto kwa njia ya kutoa elimu, ushauri na unasihi, na mbiu shawishi ili kuwa na familia na jamii bora kwa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

## Tunu zetu

- Utaalamu
- Usawa
- Uwajibikaji
- Uadilifu katika Utendaji
- Ubunifu
- Kujitolea kwa moyo
- Kujituma
- Uthabiti

## Lengo kuu

Kuhakikisha kuwa, wanandoa, wazazi wasio na wenza (single parents), vijana, watoto wa rika balehe (teenagers) wanawezeshwa na wanasaidiwa kwa Kupewa elimu ya mahusiano, afya ya uzazi, Lishe, malezi, stadi za maisha, ujasiriamali, ushauri na unasihi, na miongozo stahiki ili kuwa na familia na jamii imara.

## Wanufaika wakuu

- Watoto
- Wanawake
- Wasichana na wavulana wa rika balehe-teenagers (Umri miaka 11-19) katika maeneo ya vijijini na maeneo duni katika miji (deprived urban settings);
- Wanandoa
- Vijana na watu wazima ambao hawajaoa/ kuolewa (Umri miaka 20-45)
- Wazazi wasio na wenza-single parents (Umri miaka 16-50) wanaoishi katika mazingira magumu.

## Washirika wetu

TaMCare inafanya kazi zake kwa ushirikiano na Taasisi zingine:

- Serikali Kuu na Serikali za Mitaa
- Asasi za Kiraia zenye malengo yanayoshabihiana;
- Mashirika ya Umma
- Sekta Binafsi
- Viongozi wa Kata, Vijiji, Mitaa na Kaya
- Taasisi za dini
- Vyuo, Shule na Taasisi za Utafiti
- Vyombo vya habari.